TANGAZO LA SERIKALI Na. 501 la tarehe 21/6/2024

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16 (1))*

SHERIA NDOGO YA USIMAMIZI WA MAEGESHO NA VITUO VYA VYOMBO VYA USAFIRI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO YA MWAKA 2024

Jina

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Usimamizi wa Maegesho na Vituo vya Vyombo vya Usafiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ya Mwaka 2024.

Matumizi

**2**. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto.

Tafsiri

**3**. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chombo cha usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirishia bidhaa, abiria au mizigo;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto;

"karakana" maana yake ni eneo la Halmashauri lililotengwa kwa ajili ya shughuli za ufundi na kuhifadhi vyombo vya usafiri;

"kituo" maana yake ni eneo maalumu lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya maegesho au kwa ajili ya huduma za usafiri ambapo vyombo vya usafiri vitapakia au kushusha abiria au mizigo;

"maegesho" maana yake ni sehemu maalumu iliyotengwa kwa ajili ya kuegesha vyombo vya usafiri;

"maegesho maalumu" maana yake ni maeneo maalumu yaliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha magari chini ya uangalizi maalumu wa Halmashauri, na inajumuisha eneo la Nyerere square, pamoja na maeneo ya taasisi yanayoombewa kibali;

"stendi" maana yake ni eneo maalumu lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"ushuru wa stendi" maana yake ni malipo ya fedha taslimu kwa Halmashauri yanayolipwa na mmiliki au mfanyakazi wake kutokana na chombo chake kutumika kubeba abiria kinapoingia stendi;

"vituo vya njiani" maana yake ni vituo vyote vilivyopo pembeni ya barabara vinavyotumika kupakia na kushusha abiria ambavyo siyo stendi; na

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, shirika, taasisi au kampuni ambayo imeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi yoyote chini ya Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri.

Ushuru wa maegesho

**4**.-(1) Halmashauri itatoza ushuru wa maegesho kwa vyombo vyote vya usafiri kwa mujibu wa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Mtu mwenye chombo cha usafiri kinachoingia katika eneo lolote la maegesho atatakiwa kulipa ushuru wa maegesho kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1) na (2), vyombo vya usafiri vinavyomilikiwa na Serikali, wanadiplomasia, majeshi na magari ya kubeba wagonjwa

havitatozwa ushuru wa maegesho.

Sehemu ya maegesho

**5**.-(1) Kituo Kikuu cha mabasi, kituo cha kuegesha magari ya mizigo na maeneo mengine yaliyotengwa na Halmashauri kama maeneo ya maegesho yatakuwa ni vituo vya maegesho.

(2) Halmashauri inaweza kugawa maeneo ya maegesho kwa mistari au kwa kutumia alama yoyote itakayoonesha idadi na sehemu ambayo chombo cha usafiri kinatakiwa kuegeshwa.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (2), kukosekana kwa mistari au alama za maegesho hakutabatilisha madai ya ada ya maegesho ya chombo cha usafiri kilichoegeshwa ndani ya maeneo hayo.

Uanzishaji wa vituo vya vyombo vya usafiri

**6**. Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuanzisha vituo vya vyombo vya usafiri vinavyotoa huduma zake ndani ya Halmashauri, vinavyotoka nje ya Halmashauri na vinavyoingia ndani ya Halmashauri kwa ajili ya kubeba abiria na mizigo.

Utaratibu wa kutumia vituo vya vyombo vya usafiri

**7**.-(1) Mtu anayeendesha chombo cha usafiri hatapakia au kushusha abiria au mizigo nje ya kituo.

(2) Safari zote za mabasi zitaanza na kumalizika kwenye vituo vya mabasi isipokuwa kwa mabasi yanayopita kutoka maeneo mengine ya nje ya Halmashauri.

(3) Magari ya abiria hayataruhusiwa kusimama kwa zaidi ya dakika tano katika vituo vya njiani.

(4) Mtu ambaye hatafanya matengenezo au kuosha chombo cha usafiri katika kituo isipokuwa kwa idhini ya Halmashauri.

(5) Watumiaji wa Kituo hawataruhusiwa kuzungumza lugha ya matusi, lugha yenye kuleta uchochezi na bughudha au inayohatarisha usalama na amani ndani ya kituo.

Utaratibu wa

**8**.-(1) Halmashauri inaweza kutenga eneo la

kutenga maegesho maalumu

maegesho kuwa ni maegesho maalumu baada ya kupokea maombi kutoka kwa mtu yeyote anayetaka kutengewa eneo la kuegesha chombo cha usafiri.

(2) Katika kushughulikia maombi chini ya kanuni hii, Halmashauri itazingatia yafuatayo:

(a) athari kwa biashara au shughuli katika eneo husika endapo kibali hicho kitatolewa;
(b) uwepo wa maegesho katika eneo hilo;
(c) uwepo wa eneo mbadala la maegesho;
(d) idadi ya maeneo au nafasi zinazoombwa kuhifadhiwa;
(e) iwapo muda uliopendekezwa kwa ajili ya eneo hilo kuhifadhiwa unafaa.

(3) Endapo maombi ya kutengewa eneo la kuegesha chombo cha usafiri yatakataliwa, Halmashauri itamtaarifu mwombaji kwa maandishi na kutoa sababu za kukataa maombi hayo.

(4) Endapo maombi yatakubaliwa na mwombaji kulipa ushuru wa maegesho, Halmashauri itatoa kibali kwa ajili ya kumruhusu kutumia eneo lililotengwa bila kuingiliwa na mtu mwingine yeyote.

(5) Fomu ya maombi na kibali cha maegesho itakuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

Maegesho yasiyo rasmi

**9**.-(1) Mtu hataegesha chombo chochote cha usafiri katika maeneo ambayo hayajatengwa kwa ajili ya maegesho au kuegesha kwa namna isiyoruhusiwa.

(2) Halmashauri itazuia kwa kufunga vifaa maalumu kwenye chombo cha usafiri kilichoegeshwa vibaya au kilichoegeshwa katika eneo lisiloruhusiwa na kumtaka mmiliki au mtumiaji kulipa faini kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa na Sheria Ndogo hii.

(3) Chombo cha usafiri ambacho kitakuwa kimefungwa mnyororo au kifaa maalumu zaidi ya saa mbili bila ya kulipiwa, kitavutwa na kupelekwa kwenye karakana iliyoidhinishwa na Halmashauri kwa gharama za mwenye chombo cha usafiri, na Halmashauri haitahusika kwa namna yoyote na uharibifu utakaotokea wakati wa uvutwaji huo.

Chombo cha usafiri kilichotelekezwa

**10**.-(1) Chombo cha usafiri ambacho kitahifadhiwa katika karakana kwa muda wa siku thelathini bila kukombolewa, kitahesabika kuwa ni chombo kilichotelekezwa.

(2) Baada ya kipindi cha siku thelathini kupita, Halmashauri itawasilisha maombi mahakamani ili iweze kutamkwa kuwa chombo hicho kimetelekezwa na kutoa kibali chombo hicho kiuzwe kwa njia ya mnada wa hadhara.

(3) Kabla ya kuuzwa kwa mali yoyote iliyokamatwa chini ya kanuni ndogo ya (2), Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma kuhusu kusudio la kuuza mali hizo.

(4) Fedha itakazopatikana kutokana na mauzo ya chombo cha usafiri itatumika kulipia ushuru unaodaiwa na gharama za kukamata, na fedha itakayobaki itarejeshwa kwa mmiliki au mwakilishi wake.

Maegesho kwa muda maalumu

**11**. Magari makubwa ya mizigo yenye zaidi ya tani tano hayataruhusiwa kuegeshwa katikati ya wilaya isipokuwa kwa kibali maalumu ambacho kitalipiwa shilingi elfu ishirini kwa siku.

Usajili wa teksi, bajaji na pikipiki

**12**.-(1) Mmiliki wa teksi, bajaji au pikipiki inayofanya kazi ndani ya Halmashauri atapaswa kusajili na kulipia ada ya usajili ya chombo hicho cha usafiri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Halmashauri itatoa stika za usajili wa teksi, bajaji au pikipiki kwa kila mmiliki, na itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki kubandika stika atakayopewa na Halmashauri pembeni mwa chombo chake cha usafiri.

Uteuzi wa Wakala

**13**.-(1) Halmashauri inaweza kumteua mtu, kikundi cha watu, shirika, taasisi au kampuni kuwa Wakala wa kukusanya ushuru wa stendi kwa niaba ya Halmashauri.

(2) Wakala aliyeteuliwa chini ya kanuni ndogo ya (1) atakusanya ushuru kwa kutumia mashine ya kielekroniki.

Biashara ndogo ndogo

**14**. Mtu anayefanya biashara ndogo ndogo hataruhusiwa kufanya biashara ndani ya eneo la maegesho bila masharti, isipokuwa anaweza kukubaliana na uongozi kuhusu utaratibu wa ulinzi na usalama wa mfanyabiashara na mali na zake.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

**15**. Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kukamata na kuondoa chombo cha usafiri ambacho kimeegeshwa katika maeneo ambayo hayajatengwa kwa ajili ya maegesho au kuegesha kwa namna isiyoruhusiwa.

Makosa

**16**. Mtu ambaye-

(a) anakataa au anashindwa kulipa ushuru wa maegesho;

(b) anamshawishi mtu yeyote au kundi la watu kukataa kulipa ushuru wa maegesho;

(c) anapakia au anashusha abiria au mizigo katika eneo ambalo halikutengwa kwa ajili hiyo;

(d) anafanya matengenezo au kuosha gari katika katika sehemu iliyotengwa kwa ajili ya maegesho;

(e) anaegesha chombo cha usafiri katika eneo ambalo haliruhusiwi;

(f) anakataa kutoa taarifa au anatoa taarifa ya uongo kwa Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au wakala pale itakapohitajika;

(g) anaanzisha eneo la maegesho maalumu bila idhini ya Halmashauri; au

(h) anaegesha chombo cha usafiri nje ya mstari uliochorwa kuainisha eneo la kuegeshea chombo cha usafiri,

anatenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

kufifilisha kosa

**17**. Mkurugenzi atakuwa na mamlaka ya kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kinyume cha Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo

mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

---

JEDWALI LA KWANZA

---

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1))*

SEHEMU YA KWANZA
USHURU WA MAEGESHO MAENEO MAALUMU KWA SAA

| Na. | PEMBEZONI MWA NJIA KUU | | | ENEO MAALUM/NYERERE SQUARE | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | GARI KUBWA | GARI DOGO | CHOMBO KINGINE | GARI KUBWA | GARI DOGO | CHOMBO KINGINE |
| 1. | 500/= | 200/= | 200/= | 500/= | 500/= | 200/= |

SEHEMU YA PILI
USHURU WA MAEGESHO MAENEO MAALUMU KWA MUDA MAALUMU

(saa 12 asubuhi- 2 usiku au saa 2 usiku-saa 12 asubuhi)

| ENEO MAALUMU/NYERERESQUARE | | | |
|---|---|---|---|
| GARI KUBWA BASI/LORI) | GARI DOGO | CHOMBO KINGINE | BAJAJI/PIKIPIKI |
| 5000/= | 3000/= | 3000/= | 1000/= |

SEHEMU YA TATU

| Na. | GHARAMA YA KUFUNGA CHOMBO | | GHARAMA YA KUHIFADHI CHOMBO |
|---|---|---|---|
| 1 | Gari kubwa (Basi/Lori) | 15,000/= | 10,000/= kwa siku |
| | Gari Ndogo | 10,000/= | 5,000/= kwa siku |
| | Bajaji/Pikipiki | 5,000/= | 2,000/= kwa siku |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 8(5))*

(a) Fomu ya maombi ya maegesho maalumu: Fomu Na:…….…

MAOMBI YA MAEGESHO MAALUMU
1. Jina la mwombaji: …………………………………….
2. Anwani ya mwombaji: …………………………………
3. Namba ya simu ya mwombaji: ……………..…………
4. Ukubwa wa eneo la maegesho linaloombwa (mita za mraba) :……………
5. Eneo analoomba kwa ajili ya maegesho:
Mtaa: ..……………………barabara:……………………..Jengo Namba: ………..
6. Muda wa kibali (miezi): ……………………..…
7. Maelezo mengine (kama yapo) :…………………………………………………………………………….

Ninakiri kusoma, kuyaelewa na kukubali masharti ya kibali cha maegesho maalumu.
Jina: ………………………………………………………
Wadhifa:…………………………………………………
Saini: ………………………………………………………
Tarehe:.……………………………………………………

*Fomu hii itarudishwa katika Ofisi ya Mkurugenzi/Wakala ikiambatishwa na Stakabadhi ya ada ya maombi ya shilingi elfu ishirini (20,000) ambayo haitarejeshwa.

(b) Kibali cha maegesho maalumu
KIBALI CHA MAEGESHO MAALUMU
KIBALI Na……….
1. Jina:………………………………………………………………
2. Anwani:………………………………………………………….
3. Namba ya simu:…………… …………….……………………….
4. Namba ya stakabadhi:……………………………………………
5. Ofisi iliyotoa kibali:……………………………………………….
6. Eneo lilipo:
Mtaa:..……………barabara:……….………..Jengo:………………
7. Ukubwa wa eneo la maegesho (mita za mraba):……………….
8. Kiasi kilicholipwa kwa miezi ……… Jumla ya sh……………….
9. Muda wa kibali…………kuanzia…….……..…hadi……………..
10. Maelezo mengine yatakayohitajika (kama yapo):…………………….………………..

Kimetolewa tarehe…………...……mwezi……….…………….mwaka……………, 2024

Kimetolewa na:-
Jina:……………………..……………………………………………………
Cheo:………………………………………………………………….…….

*Tangazo la Serikali Na.501 (Linaendelea.)*

Saini:……………………………..………… Muhuri wa Ofisi:.……………

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 17)*

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi....................................................................nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ....................................................................ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, kwamba mnamo tarehe..........ya mwezi.......................Mwaka...........................nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kanuni ya..............ya Sheria Ndogo ya Usimamizi wa Maegesho na Vituo vya Vyombo vya Usafiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ya Mwaka 2024.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, niko tayari kulipa kiasi cha ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU NA KADRI YA UFAHAMU WANGU.
Leo tarehe.....................ya Mwezi.........................Mwaka.....................................
Jina.................................................. Saini...........................................................

MBELE YANGU:
Jina:......................................................
Wadhifa:....................................................
Saini.........................................................
Tarehe.......................................................

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto imebandikwa katika hizi Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kufuatia Azimio la kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kilichofanyika tarehe 12/5/2023 na kushuhudiwa,

Lakiri imebandikwa mbele ya:-

IKUPA H. MWASYOGE,
*Mkurungenzi mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Lushoto*

MATHEW MBARUKU,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya wilaya,*
*Lushoto*

**NAKUBALI**,

L.S

Dodoma,
25 Machi, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB.),
*Waziri wa Nchi -OR-Tamisemi*,